# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MWAUKOLI,
S.L.P. 247,
**MWANHUZI – MEATU.**
15 – 12 – 2020.

**Kumb. Na. MSS/ADM/VOL.II/020/07.**

Ndugu: -

________________________________________

________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWAUKOLI MWAKA 2021:**

### 1.0 UTANGULIZI
Ninafurahi kukutaarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mwaukoli. kujiunga Shule inapatikana wilaya ya Meatu, mkoa wa Simiyu. Ipo umbali wa kilomita 104 kutoka mji wa Mwanhuzi (makao makuu ya wilaya ya Meatu).

### 1.1 KUFUNGUA SHULE
Shule itafunguliwa tarehe **11 – 01 – 2021**, unatakiwa kufika shuleni siku hiyo kwani masomo yataanza mara moja shule itakapofunguliwa. Usiporipoti ndani ya siku kumi nne (14) tangu shule kufunguliwa, utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

### 2.0 MASHARTI YA KUJIUNGA NA KUENDELEA NA MAFUNZO
Unatakiwa kutimiza yafuatayo: -

- ✓ Kupimwa na Daktari wa Serikali katika hospitali ya wilaya (Mwanhuzi),au kituo cha afya Mwandoya ili akuthibitishe kuwa unafaa kuendelea na mafunzo ya Elimu ya Sekondari (Request for Medical Examination) imeambatishwa.

### 3.0 SARE YA SHULE
#### 3.1 Wavulana
- ✓ Suruali mbili **za DARK BLUE** zisizobana (siyo modo), mashati mawili meupe ya mikono mifupi (unashauriwa kununua mashati imara ya mitumba).
- ✓ Tai ndefu ya dark blue.
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika, visigino vifupi na soksi fupi nyeusi jozi mbili.
- ✓ **Mkanda wa suruali wa rangi nyeusi, mikanda yenye vyuma vikubwa hairuhusiwi, ukikutwa umevaa na sare ya shule utanyang'anywa).**

#### 3.2 Wasichana
- ✓ Sketi mbili, ndefu zinazofunika kifundo cha mguu za rangi ya **DARK BLUE,** zenye marinda manane (rinda box), mashati mawili meupe ya mikono mifupi (unashauriwa kununua mashati imara ya mtumba).

- ✓ Tai ndefu ya rangi ya dark blue (unaposhona sketi msisitize fundi akushonee na tai).
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika, visigino vifupi na soksi ndefu nyeusi jozi mbili.

### 3.3 Sare ya Michezo na Kazi za Mikono

- ✓ Traka ya BLUU kwa wavulana na wasichana.
- ✓ T shirt ya rangi ya kijivu .
- ✓ Raba rangi nyeusi au nyeupe.

## 4.0 VIFAA VYA KUJA NAVYO

### 4.1 Vifaa Binafsi: -

- ✓ Madaftari makubwa (Kaunta - 3 Quire) kumi (10) na kalamu za kutosha.
- ✓ Mkebe wa Hisabati (Mathematical Set).
- ✓ Mkoba wa kubebea madaftari kama begi la mgongoni ..
- ✓ Mwanafunzi anayetoka kijiji cha mbali, mzazi/mlezi amwandalie baiskeli yake atakayotumia shuleni siku zote.

.

## 5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE ZA SEKONDARI

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi na ile ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mwanafunzi anapaswa kuzitii na kuziishi.

### 5.1 Sheria na Kanuni za Shule za Sekondari

- ✓ Mwanafunzi anapaswa kusimama na kumsalimia Mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
- ✓ Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wao.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kwa Mwanafunzi mwenzake, Mwalimu, na kwa mtu mwingine.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo: -
  - ➢ Kuvuta sigara.
  - ➢ Kufuga kucha, kufuga ndevu na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
  - ➢ Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.
  - ➢ Kugombana.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, na Fedha za Taifa.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kumudu kuimba vizuri nyimbo zifuatazo: -
  - ➢ Wimbo wa Taifa,
  - ➢ Wimbo wa Tanzania Tanzania,
  - ➢ Wimbo wa Tazama Ramani, na
  - ➢ Wimbo wa Shule.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo, ndani na nje ya darasa muda wote wa masomo.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria katika kazi/shughuli zote za mikono.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria katika mikutano ya shule kama BARAZA la shule, Ukaguzi wa usafi, Kupandisha Bendera ya Taifa, n.k.



Scanned with CamScanner

- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyo katika ratiba ya kila siku.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia wito wa DHARURA.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote anapokuwa shuleni na wakati: -
  - ➢ Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughulli za kishule.
  - ➢ Wanafunzi wanapofanya maandamano.
  - ➢ Wa BARAZA la shule.
  - ➢ Mwanafunzi atavaa nguo za michezo wakati wa michezo tu.
  - ➢ Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo haviruhusiwi kuvaliwa pamoja na sare ya shule.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalum.

- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo, isipokuwa kwa kibali maalum: -
  - ➢ Ofisi za shule na Maabara.
  - ➢ Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo: -
  - ➢ Vilabu vya pombe (bar) na nyumba za kulala wageni.
  - ➢ Kumbi za starehe (kumbi za video & saluni kuangalia video).

### 5.2 Makosa Yanayoweza Kusababisha Mwanafunzi Kufukuzwa Shule

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, n.k.
4. Makosa ya jinai.
5. Kupiga na kupigana.
6. Kuharibu kwa makosudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
10. Kutoa miimba.
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.

## 6.0 HITIMISHO

Ni matumaini yetu kuwa umeipokea nafasi hii kwa furaha,

**"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWAUKOLI"**

Asante,

……………………

**WILLIAM M. KUDOJA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI MWAUKOLI S.L.P. 247 MEATU.

Afisa Elimu Sekondari,
S.L.P. 44,
**MWANHUZI – MEATU.**



Scanned with CamScanner

MEATU DISTRICT COUNCIL
MWAUKOLI SECONDARY SCHOOL

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**To: -**

The Medical Officer,
Meatu District Hospital,
P.O. Box 25,
**MWANHUZI – MEATU.**

**Form: -**

The Headmaster,
Mwaukoli Secondary School,
P.O. Box 247,
**MWANHUZI – MEATU.**

Please examine ______________________ (insert name) as *she/he is able to join a Secondary Education Programme. Please write (NO) in the appropriate place, if (YES) indicate diagnosis: -

1. Height: ______________________
2. Weight: ______________________
3. Skin Disease: ______________________
4. Eyes:
   - Sight Without Glasses: Right: ______________ Left: ______________
   - Pupils: - Right: ______________ Left: ______________
5. Please state Condition of Ears (if any discharge):
   - Right: ______________ Left: ______________
6. Cardiovascular System:
   - Blood Pressure: Systolic: ______________ Diastolic: ______________
   - Heart(any tumour): ______________________
7. Abdomen:
   - Hernia: ______________________
   - Hydrate: ______________________
   - Liver: ______________________
   - Kidneys: ______________________
8. Any Other Clinical (state diagnosis): ______________________

______________________________________________

______________________________________________

## MEDICAL CERTIFICATE
### (TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have personally examined the above mentioned and consider that, *she/he *is/is not physically fit to join the above course.

Name: ______________________ Designation: ______________________

Signature: ______________________ Date: ______________________

Official Stamp: ______________________



Scanned with CamScanner